# KATIBA YA

## CHAMA CHA KUTETEA HAKI NA MASILAHI YA WALIMU TANZANIA

# (CHAKAMWATA)

True Copy.

CHAMA CHA KUTETEA HAKI NA MASILAHI YA WALIMU TANZANIA
KATIBU MKUU
(CHAKAMWATA)

S. L. P. 2801

MBEYA

TOLEO LA KWANZA MEI, 2012

# KATIBA YA CHAMA CHA KUTETEA HAKI NA MASILAHI YA WALIMU TANZANIA (CHAKAMWATA)

*Mpangilio wa Ibara*


**SURA YA KWANZA**

UFAFANUZI KUHUSU CHAKAMWATA

1. Utangulizi
2. Jina la Katiba ya Chama
3. Anuani ya Makao Makuu ya CHAKAMWATA
4. Motto wa CHAKAMWATA
5. Ofisi ya Makao Makuu ya CHAKAMWATA-Taifa
6. Tafsiri ya Maneno Mbalimbali

**SURA YA PILI**

MADHUMUNI NA MISINGI YA CHAKAMWATA

7. Madhumuni ya CHAKAMWATA

**SURA YA TATU**

AINA ZA WANACHAMA NA SIFA ZA KUJIUNGA NA CHAKAMWATA

8. Aina za Wanachama wa CHAKAMWATA
9. Sifa za kuwa Mwanachama wa CHAKAMWATA

**SURA YA NNE**

MASHARTI YA KUJIUNGA, WAJIBU NA HAKI ZA MWANACHAMA WA CHAKAMWATA

10. Masharti na vigezo vya Kujiunga na CHAKAMWATA
11. Wajibu wa Mwanachama wa CHAKAMWATA
12. Haki za Mwanachama wa CHAKAMWATA

**SURA YA TANO**

UKOMO WA MWANACHAMA WA CHAKAMWATA

13. Ukomo wa kuwa Mwanachama wa CHAKAMWATA

**SURA YA SITA**

MUUNDO WA UONGOZI, SIFA, KAZI NA MADARAKA YA VIONGOZI WA CHAKAMWATA

14. Sifa za kuwa Kiongozi wa CHAKAMWATA
15. Muundo wa uongozi wa CHAKAMWATA
16. Mgawanyo wa Kanda za kiuongozi
17. Kazi na Madaraka ya Viongozi wa CHAKAMWATA
18. Kamati Tendaji za CHAKAMWATA
19. Kamati ya Nidhamu ya CHAKAMWATA

20. Kazi na Madaraka ya Kamati ya Nidhamu
21. Kamati ya Ukaguzi ya CHAKAMWATA
22. Kazi na Madaraka ya Kamati ya Ukaguzi
23. Ukomo wa Uongozi wa chama cha CHAKAMWATA

**SURA YA SABA**

MIKUTANO MBALIMBALI YA CHAKAMWATA

24. Kuwepo kwa Mikutano ya CHAKAMWATA
25. Muainisho wa Mikutano mbalimbali na Maamuzi yake
26. Kazi za mkutano Mkuu,
27. Kuitisha Mgomo na Maeneo ya Migomo

**SURA YA NANE**

BODI YA WADHAMINI WA CHAKAMWATA

28. Bodi ya Wadhamini wa CHAKAMWATA
29. Upatikanaji wa Bodi ya Wadhamini
30. Sifa za kuwa Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini
31. Vikao vya Bodi ya Wadhamini wa CHAKAMWATA
32. Majukumu ya Bodi ya Wadhamini wa CHAKAMWATA
33. Ukomo wa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini

**SURA YA TISA**

MFUKO MKUU, FEDHA NA VYANZO VYA MAPATO YA CHAKAMWATA

34. Utunzaji wa fedha na Mali za CHAKAMWATA
35. Vyanzo vya Mapato ya CHAKAMWATA
36. Akaunti ya Benki ya CHAKAMWATA
37. Matumizi ya fedha za CHAKAMWATA

**SURA YA KUMI**

MAREKEBISHO YA KATIBA NA KANUNI ZA CHAKAMWATA

38. Marekebisho ya Katiba pamoja na Kanuni zake
39. Hoja zinazohusu Marekebisho ya Katiba.
40. Maamuzi ya Hoja za Marekebisho ya Katiba.

**KUFUTWA KWA CHAMA CHA CHAKAMWATA**

41. Sababu za kutofutwa kwa CHAKAMWATA.
42. Sababu za kufutwa kwa CHAKAMWATA.
43. Mgawanyo wa mali za CHAKAMWATA.
44. AKIDI ya maamuzi ya Mkutano wa kukifuta CHAKAMWATA.

## UTANGULIZI

Chama cha Kutetea Haki na Masilahi ya Walimu Tanzania (CHAKAMWATA), ni utambulisho wa Chama cha hiari cha Wafanyakazi ambao ni Walimu. CHAKAMWATA kinaundwa na Walimu ambao wana elimu ya ngazi ya astashahada (cheti), stashahada (Diploma), shahada (Degree), shahada ya uzamili (Masters) na shahada ya uzamifu (PhD). Walimu wote wanaofundisha darasani katika shule za chekechea, shule za awali, shule za msingi, shule za sekondari, vyuo vya kati, vyuo vikuu pamoja na walimu wanaofanya kazi za kuteuliwa maofisini hawatungi sera wala kuingia mikataba na wafanyakazi kwa niaba ya mwajiri.

Kwa kuwa sisi ni walimu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunalo jukumu kubwa la kusimamia na kutekeleleza Mitaala kwa kuelimisha Umma na kuandaa wataalamu wa leo na wa kesho wa nchi hii.Vilevile elimu inahitaji ujuzi, ufahamu, uelewa, uadilifu na upendo pamoja na utafiti wa kina ili kutoa elimu bora.

Walimu kwa pamoja tumeazimia kuungana na kuunda chama chetu kinachoitwa Chama cha Kutetea Haki na Masilahi ya Walimu Tanzania (CHAKAMWATA), ili kuhakikisha kuwa walimu wote, tunapata haki zetu zote za msingi tunazostahili kutoka kwa waajiri wetu, baada ya kutimiza wajibu wetu kwa mujibu wa kununi na sheria zinazotawala utumishi wetu. Pia ili kuhakikisha kuwa Elimu na taaluma ya Ualimu inatambuliwa na kuheshimiwa na watu wote wakijua kuwa Ualimu ni taaluma mama ya taaluma zote, kwa kuwa hakuna msomi mahiri yeyote na wa utaalamu wowote ambaye anaweza kufikia hatua ya kuitwa msomi au mtaalamu wa jambo fulani bila kupitia mikononi mwa mwalimu.

CHAKAMWATA kinaamini kuwa ili kiongozi aweze kupigania na kutetea haki na masilahi ya walimu vizuri na kwa ukamilifu, ni sharti yeye mwenyewe awe ni mwalimu aliyeajiriwa ili aweze kupata hisia na vionjo halisi vya kuonewa, kubaguliwa, kudhulumiwa, kunyanyaswa na kupuuzwa na mwajiri. Na hivyo kuona kuwa kero wanazozipata walimu nchini ni kero anazozipata yeye pia. Kiongozi wa CHAKAMWATA ambaye si mwalimu kwa kuajiriwa kamwe hawezi kuwapigania na kuwatetea walimu kikamilifu na ni rahisi kuwasaliti walimu kwani kero za walimu si kero zake. CHAKAMWATA kinaamini kuwa ni katika nguvu ya Umoja tu, walimu wote nchini twaweza kufikia ukombozi halisi kifikra na kimtazamo, kiuchumi, kijamii na kisiasa.

CHAKAMWATA ni chama cha hiari kisicho cha kujipatia kipato, faida au masilahi yoyote binafsi na kitaendesha shughuli zake kwa haki kwa manufaa na masilahi ya umma wa walimu wote. Mwanachama na kiongozi yeyote wa chama ambaye pia ni mwalimu, afahamu kwamba kwa kiasi kikubwa atakitumika chama kwa kujitolea na atajengewa uwezo kwa sehemu kulingana na uwezo wa chama kiuchumi.

Katiba hii imeandaliwa kwa kufuata misingi, kanuni na sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 20 Ibara ndogo ya 1 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Pia kwa kuzingatia kifungu cha 9 (1) (a), (b) cha sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini namba 6 ya Mwaka 2004.

## SURA YA KWANZA

## UFAFANUZI KUHUSU CHAKAMWATA

**Jina la Chama**

**1.**(1) Jina la Chama hiki litakuwa**"Chama cha Kutetea Haki na Masilahi ya Walimu Tanzania"**kwa kifupi **CHAKAMWATA.**

**Jina la Katiba ya Chama**

(2) Katiba hii itajulikana kama Katiba ya Chama cha Kutetea Haki na Masilahi ya Walimu Tanzania (CHAKAMWATA) ya mwaka 2012.

**Kazi za CHAKAMWATA**

(3) CHAKAMWATA kitapigania na kutetea ustawi, haki na masilahi bora ya wafanyakazi ambao ni walimu, kutetea ubora wa elimu nchini ili kujenga Taifa la wasomi weledi na wenye uzalendo kwa nchi yao. Pia kuwashauri waajiri ili kuboresha mazingira ya kazi na maslahi ya **walimu**.

**Kanuni za Chama cha CHAKAMWATA**

(4) Katiba hii itasomwa pamoja na Kanuni zitakazoundwa na Kamati ya Katiba kwa kushirikiana na Kamati ya Nidhamu na Kamati kuu ya Taifa na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa CHAKAMWATA. Pale ambapo Kanuni zitaonekana kutokubaliana na Katiba, basi Katiba ya CHAKAMWATA ndiyo itakayosimama na zingatiwa zaidi.

(4)Katiba hii itatumika ndani ya nchi ya Tanzania katika maeneo yote ya kazi, Matawi yote yaliyosajiliwa, Halmashauri za Wilaya zote zilizosajiliwa kwa mujibu wa Katiba hii, Mikoa na Kanda zote zinazotambuliwa kwa mujibu wa Katiba hii, hadi Taifa.

**Anuani ya CHAKAMWATA**

**2.** Anuani ya Makao Makuu ya CHAKAMWATA itakuwa ni:-

**KATIBU MKUU,**
**CHAMA CHA KUTETEA HAKI NA MASILAHI**
**YA WALIMU TANZANIA (CHAKAMWATA),**
**S. L. P. 2801,**
**MBEYA**

**Motto wa CHAKAMWATA**

**3.** Motto wa **CHAHAMWATA** utakukuwa ni huu:-

***"Kazi na Haki ni Msingi wa Maendeleo"***

**Makao Makuu ya CHAKAMWATA**

**4.** (1) Makao Makuu ya CHAKAMWATA kwa sasa yatakuwa mkoani Mbeya.

(2) Mkutano Mkuu unaweza kupendekeza na kupitisha mabadiliko ya ofisi kuu/ Makao Makuu wakati wowote itakapobidi kama kuna haja ya kufanya hivyo.

## TAFSIRI YA MANENO

5. (1) Katika Katiba hii ya CHAKAMWATA , ila iwapo maelezo yanahitaji vinginevyo kutakuwa na tafsiri ya maneno kama hii:-

**Tafsiri ya Maneno Mbalimbali**

**"Bodi ya wadhamini"** maana yake ni watu walio dhamini Chama ikiwemo Katiba, Kanuni na hati nyinginezo pamoja na Mali za Chama.

**"Cheti"** maana yake ni: Tunu aliyoipata mwalimu aliyehudhuria mafunzo ya kazi ya ualimu kwa muda usiopungua miaka miwili na kufaulu Mtihani wa Baraza la Mitihani la Taifa.

**"Gawio"** ni kiasi cha fedha kinachotokana na **FAIDA** ipatikanayo kutoka kwenye mradi au kitega uchumi kinachofanya biashara kwa mafanikio endapo kitakuwepo, kiasi hicho atapewa Mwalimu anapostaafu kama shukurani ya chama kwa mwanachama wake kwa kukichangia chama kwa muda wa utumishi wake. Kanuni ya kukokotoa gawio hilo itaandaliwa na mradi kwa kushirikiana na Kamati kuu ya Taifa na kupitishwa na mkutano mkuu.

**"Halmashauri"** maana yake ni eneo lote linalosimamiwa na Mkurugenzi Mtendaji kama mwajiri wa Walimu kwa niaba ya serikali.

**"Halmashauri ya Wilaya"** maana yake ni ngazi ya pili ya Uongozi wa CHAHAMWATA Kutoka ngazi ya Kata.

**"Kanda"** maana yake ni eneo linalijumuisha Mkoa mmoja au zaidi ya utawala wa kiserikali.

**"Kanuni za CHAKAMWATA"** maana yake ni sheria ndogo ndogo (by laws) zinazofafanua Katiba ya CHAKAMWATA na ambazo zinatoa mwongozo na kutawala utendaji na utendekaji wa kila siku wa shughuli za CHAKAMWATA.

**"Katiba ya CHAKAMWATA"** maana yake ni muongozo mkuu unaobeba taratibu zote za uendeshaji wa Chama na hivyo kuzingatiwa kama sheria kuu ya CHAKAMWATA.

**"Michango"** maana yake ni makato au malipo ya kila mwezi kutoka kwenye mshahara wa kila mwezi wa mwalimu mwanachama wa CHAKAMWATA ambao ni asilimia 1% ya mshahara wake wa kila mwezi.

**"Mratibu wa Kanda"** maana yake ni Kiongozi anayesimamia shughuli za CHAKAMWATA kwa kila Kanda kwa mujibu wa Katiba hii na Kanuni zake.

**"Mratibu wa Mkoa"** maana yake ni Kiongozi anayesimamia shughuli za CHAKAMWATA kwa kila Mkoa kwa mujibu wa Katiba hii na Kanuni zake.

**"Mwalimu"** Maana ya kwanza ya Mwalimu; Ni mtu yeyote aliyesomea ualimu kuanzia ngazi ya astashahada (cheti), stashahada (Diploma), shahada (Degree) na shahada ya uzamili (Masters) na shahada ya uzamifu (PhD) na kuendelea. Mwalimu yeyote anayefundisha katika shule za

chekechea, shule za awali, shule za msingi, shule za sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu pamoja na walimu wanaofanya kazi za kuteuliwa maofisini.

Maana ya pili ya mwalimu; Ni mtu yeyote ambaye hakusomea ualimu katika vyuo vya elimu, lakini kutokana na weledi wake katika taaluma na utaalamu aliosomea, amekubalika na taasisi inayotambulika kisheria kufanyakazi ya ualimu kwa kufundisha na kutoa elimu na maarifa kwa wanafunzi wanaosomea taaluma na utaalamu mwingine mbali na ualimu kama vile utabibu, uhandisi, uchumi, biashara, n.k. ambaye kwa hiari yake mwenyewe anaamua kujiunga na Chama cha CHAKAMWATA baada ya kuona na kujiridhisha juu ya CHAKAMWATA kuwa ni chama sahihi kwake kujiunga nacho ili kupigania, kulinda na kutetea Haki zake na maslahi yake.

**"Mwanachama wa CHAKAMWATA"** maana yake ni Mwalimu aliyesajiriwa ndani ya Chama hiki.

**"Shahada"** maana yake ni tunu aliyotunukiwa mwalimu baada ya kuhudhuria mafunzo ya Ualimu ya Chuo Kikuu na kuhitimu kwa mafanikio.

**"Shahada ya uzamili"** maana yake ni tunu aliyotunukiwa mwalimu baada ya kuhudhuria mafunzo ya ualimu ya Chuo Kikuu kwa mara ya pili na kuhitimu kwa mafanikio.

**"Shahada ya uzamifu"** maana yake ni tunu aliyotunukiwa mwalimu baada ya kuhudhuria mafunzo ya ualimu ya Chuo Kikuu kwa mara ya tatu na kuhitimu kwa mafanikio.

**"Stashahada"** maana yake ni tunu aliyotunukiwa mwalimu baada ya kuhudhuria mafunzo ya ualimu ya chuo cha ngazi ya kati na kuhitimu kwa mafanikio.

**"Tasnia"** maana yake ni Nyanja, taaluma au utaalamu wa.

**"Tasnia ya Elimu"** maana yake ni taaluma au utaalamu katika fani ya elimu.

**"Tawi"** maana yake ni ngazi ya CHAKAMWATA inayohusisha eneo lote la Kata, kwa kujumuisha wanachama na viongozi wake wote.

**"CHAKAMWATA"** ni Chama cha Wafanyakazi ambao ni Walimu wanaofundisha katika taasisi za elimu za serikali, mashirika ya dini na taasisi za watu binafsi pamoja na wanaofanyakazi za kuteuliwa maofisini lakini ambao hawafanyi kazi ya kutunga sera na kuingia mikataba na wafanyakazi kwa niaba ya mwajiri. Kwa hiyo huu ndiyo utambulisho pekee kwa jina la Chama cha Kutete Haki na Masilahi ya Walimu Tanzania.

**"Viongozi wa CHAKAMWATA"** maana yake ni walimu waliochaguliwa au kuteuliwa na walimu wenzao na kukabidhiwa dhamana ya kuongoza na kusimamia shuguli za kila siku za

CHAKAMWATA.

**"Viongozi Waandamizi wa CHAKAMWATA au Kamati Tendaji ya CHAKAMWATA"** maana yake ni Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Mtunza Hazina wote kwa pamoja, pamoja na Mratibu wa Mkoa na Mratibu wa Kanda.

**"Wanachama waanzilishi"** maana yake ni walimu waliokaa pamoja na kwa nia moja, kwa mara ya kwanza wakaamua kuanzisha chama cha wafanyakazi cha CHAKAMWATA na Orodha ya majina yao imeoneshwa kwenye kumbukumbu.

**"Wanachama wanaojiunga"** maana yake ni walimu ambao hawakushiriki kuanzisha chama cha CHAKAMWATA lakini baadaye na kwa hiari yao wenyewe wamejaza fomu maalum ya kuomba kujiunga na CHAKAMWATA, wakaruhusiwa, na hivyo wakajiunga na kutoa michango ya kila mwezi michango.

(2) Bila kuathiri Katiba hii kutakuwa na Kanuni mbalimbali za CHAKAMWATA zitakazotungwa na Kamati ya Katiba kwa kushirikiana na Kamati ya Nidhamu na Kamati kuu Taifa na kupitishwa na Mkutano Mkuu. Kanuni hizo zitaitwa *Kanuni za Kudumu za CHAKAMWATA*

## SURA YA PILI

## MADHUMUNI NA MISINGI YA CHAKAMWATA

**Madhumuni ya CHAKAMWATA**

**6**-(1) CHAKAMWATA kitakuwa na Madhumuni haya:-

(a) Kuwaunganisha walimu wote nchini ili kuwa na nguvu na kauli ya pamoja tukiwa ni wataalamu, katika mambo yahusuyo wajibu na haki zetu katika ajira zetu.

(b) Kuwaongoza walimu katika kutetea na kudai haki mbalimbali na masilahi bora tunayostahili kutoka kwa waajiri wetu baada ya kuwa tumetimiza wajibu wetu.

(c) Kuwawakilisha walimu mbele ya waajiri wao katika kutetea na kudai haki mbalimbali na masilahi bora wanayostahili kutoka kwa waajiri wetu baada ya kuwa wametimiza wajibu wao.

(d) Kuwahamasisha na kuwaelimisha Walimu ili waweze kujua haki zao zinazotokana na kutimiza wajibu wao kwa nafsi zao, kwa jamii, kwa waajiri wao na kwa Taifa lao popote pale walipo pamoja na kuzitambua, kuzipigania, kuzitetea, kuzihifadhi na kuzilinda haki zao.

(e) Kurahisisha ufikiwaji wa huduma mbalimbali kutoka kwa wadau wengine wa elimu na maendeleo kutoka katika sekta mbalimbali nchini.

(f) Kushirikiana na kuungana na vyama mbalimbali

vinavyopigania maendeleo, haki na Masilahi ya walimu vya ndani na nje ya nchi.

(g) Kufanya mawasiliano na waajiri ambao ni serikali, mashirika ya dini na watu binafsi kwa niaba ya walimu kuhusu haki na maslahi mbalimbali ya walimu ambayo hayakutolewa kwa wakati, kwa kadiri mwalimu mmoja mmoja au walimu zaidi ya mmoja watakavyofikisha malalamiko yao kwa chama.

(h) Kujenga hoja za kupinga sheria, sera na nyaraka mbalimbali zinazotolewa na waajiri ambazo zinalenga kukiuka na kukandamiza haki za walimu na kuzorotesha masilahi ya walimu nchini.

(i) Kufanya tafiti mbalimbali kuhusu matatizo mbalimbali yanayowakabili walimu wanapotekeleza majukumu yao na kutoa ushauri kwa serikali na wadau wengine wa elimu kwa manufaa na ustawi wa Taifa letu.

(2)Kuweka uhusiano mzuri kati ya mwajiri na mwajiriwa katika mazingira ya kazi.

(3) Kuwasaidia walimu ili waweze kujitambua na kujua thamani na nafasi yao katika maendeleo na ustawi wa Taifa.

(3) Kuwahamasisha walimu ili waipende kazi yao ya Ualimu.

## SURA YA TATU

## WANACHAMA WA CHAKAMWATA

**Aina za Wanachama wa CHAKAMWATA**

**7.** (1) Chama cha Kutetea Haki na Masilahi ya Walimu Tanzania (**CHAKAMWATA)** kitakuwa na wanachama wa aina mbili ambao ni hawa wafuatao:-

(i) Wanachama waanzilishi.

(ii) Wanachama wanaoomba kujiunga.

(2) Kwa mujibu wa Ibara7 (1) ya Katiba hii wanachama wote watakuwa na haki sawa.

## SIFA ZA KUJIUNGA NA CHAMA CHA KUTETEA HAKI NA MASILAHI YA WALIMU TANZANIA (CHAKAMWATA)

**Sifa za kuwa Mwanachama wa CHAKAMWATA**

**8.** Sifa za kuwa mwanachama wa CHAKAMWATA zitakuwa ni:-

(i) Awe ni mwalimu kitaaluma kuanzia ngazi ya astashahada (cheti), stashahada, shahada, shahada ya uzamili, shahada ya uzamifu na kuendelea.

(ii) Awe ameajiriwa na serikali, sekta binafsi ndani ya nchi na ambaye bado hajapata ajira lakini anatafuta ajira ya Ualimu

ndani ya nchi ya Tanzania.

(iii) Kwa mtu ambaye si mwalimu kitaalum, basi awe ni mtu aliyekubalika kufanyakazi ya ualimu kutokana na umuhimu na kuhitajika kwa weledi wake katika taaluma na utaalamu aliosomea, katika taasisi inayotambulika kisheria

(iv) Awe ni mtu anayependa kuwajibika bila kusukumwa na awe na moyo wa kujitolea.

(v) Awe na uwezo wa kutunza siri za CHAKAMWATA.

(vi) Awe raia wa Tanzania wa Kuzaliwa au wa Kuandikishwa au mgeni aliyepata kibali kutoka mamlaka za nchi cha kufanyakazi ya ualimu nchini.

(vii) Awe tayari kukitumikia CHAKAMWATA kwa kuhudhuria vikao na mikutano inapoitishwa.

(viii) Awe tayari kusimamia maamuzi ya chama nyakati za kuunganisha nguvu ili kudai haki za walimu kutoka kwa waajiri.

(ix) Awe tayari kwa maelekezo ya chama, kuungana na walimu wenzake wanaodhulumiwa ili kudai haki zao hata kama yeye mwenyewe hana madai kama hayo, na atafanya hivyo ili kulinda na kutetea haki na masilahi endelevu ya walimu kwa ujumla na hivyo kuifanya kazi na taaluma ya ualimu kuheshimika.

## SURA YA NNE

## MASHARTI YA KUJIUNGA, WAJIBU NA HAKI ZA MWANACHAMA WA CHAKAMWATA

**Namna ya kujiunga, kuwa Mwanachama wa CHAKAMWATA**

**9.** Kila mwanachama wa CHAKAMWATA bila kuathiri Ibara 8 ya Katiba hii atalazimika kuzingatia Masharti na vigezo vifuatavyo ili kujiunga na chama:-

(a) Kwa hiari yake mwenyewe, atajaza fomu maalumu ya kisheria inayoitwa TUF.6 na kuikabidhi moja kwa moja kwa uongozi wa halmashauri aliyopo au kwa uongozi wa tawi lake au kwa mjumbe wa chama aliye kwenye kituo chake cha kazi.

(b) Awe na akili timamu.

## WAJIBU WA MWANACHAMA WA CHAKAMWATA

**Wajibu wa Mwanachama wa CHAKAMWATA**

**10.** Kila mwanachama wa Chama cha Kutetea Haki na Masilahi ya Walimu Tanzania (CHAKAMWATA) atawajibika kwa mujibu wa Katiba hii kwa:-

(a) Kutoa michango yote iliyoidhinishwa na CHAKAMWATA.

(b) Kulinda na kutetea Katiba ya CHAHAMWATA.

(c) Kushiriki kikamilifu katika kutekeleza madhumuni ya CHAKAMWATA.
(d) Kutunza siri za CHAKAMWATA.
(e) Kuwajibika ndani ya CHAKAMWATA.
(f) Kuhamasisha Wanachama wa chama hiki kuhudhuria mikutano na vikao vya CHAKAMWATA vinapoitishwa.
(g) Kushauriana na kushirikiana na wanachama wenzake wa wa CHAKAMWATA popote pale alipo kwa ajili ya masilahi yao na Taifa.
(h) Kuhudhuria vikao na mikutano yote ya CHAKAMWATA anayotakiwa kuhudhuria.

### HAKI ZA MWANACHAMA WA CHAKAMWATA

**Haki za Mwana chama wa CHAKAMWATA**

**11.** Kila mwanachama wa CHAKAMWATA atakuwa na haki zilizoainishwa ndani ya Katiba hii ambazo ni:-

(a) Kumchagua kiongozi amtakaye au yeye mwenyewe kuchaguliwa katika nafasi mbalimbali za uongozi.
(b) Kupata na kujua taarifa za maendeleo yoyote ndani ya CHAKAMWATA.
(c) Kupata maslahi/fedha/gawio wakati wa kustaafu kazi kama shukurani za Chama kwa mwanachama wake kulingana na taratibu za CHAKAMWATA iwapo kutakuwa na vitega uchumi vinavyoendeshwa kwa mafanikio.
(d) Kujulishwa jambo lolote ndani ya CHAKAMWATA kwa kufuata kanuni za CHAKAMWATA.
(e) Kusimamiwa na Chama cha CHAKAMWATA katika vyombo vya Sheria iwapo mwajiri wake anamdhulumu au anakataa kumpatia mwajiriwa wake haki na stahili zake halali.
(f) Kila mwanachama wa Chama cha Kutetea Haki na Masilahi ya WalimuTanzania (CHAKAMWATA) atakuwa na haki ya kupata gawio ambalo litatokana na miradi ya uwekezaji na vitega uchumi vinaavyojiendesha kwa mafanikio kama vitakuwepo. Gawio hilo litakuwa ni shukurani ya chama kwa mwanachama wake kwa kukichangia chama kwa muda wa utumishi wake. Gawio hili atapewa wakati wa kustaafu kazi kwa mwajiri wake. Kama atafariki kabla ya kustaafu, basi warithi wake watapewa gawio hilo kama ambavyo angestahili mstaafu. Aidha endapo mwanachama ataacha au kuachishwa kazi na mwajiri wake kwa sababu nyingine yoyote, haki zake zilizo ndani ya CHAKAMWATA hazitapotea.
(g) Kutoa mchango wake wa mawazo, kusikilizwa, kuthaminiwa na kuheshimiwa mawazo yake katika vikao na mikutano.

(h) Mwalimu atakayefukuzwa uanachama kwa makosa mbalimbali yaliyothibitika ikiwa ni pamoja na uvunjaji wa makusudi wa Katiba na Kanuni za CHAKAMWATA, ubadhirifu wa fedha na ufujaji wa mali za chama, atakuwa amepoteza haki zake zote zilizokuwa ndani ya chama.

## SURA YA TANO

## UKOMO WA MWANACHAMA WA CHAMA CHA KUTETEA HAKI NA MASILAHI YA WALIMU TANZANIA (CHAKAMWATA)

**Ukomo wa Mwana chama wa CHAKAMWATA**

**12.**(1) Sababu zifuatazo zinaweza kumfanya mwalimu ambaye ni mwanachama wa Chama cha Kutetea Haki na Masilahi ya Walimu Tanzania (CHAKAMWATA), akome kuwa mwanachama

(a) Kutoshiriki vikao vya CHAKAMWATA kwa mwaka mzima bila taarifa yoyote ya sababu ya kutohudhuria kuufikia Uongozi wa ngazi husika.
(b) Kukiuka kwa makusudi Masharti ya Katiba ya CHAKAMWATA.
(c) Kusimamishwa Uanachama wa CHAKAMWATA na Mkutano Mkuu.
(d) Kufariki dunia kwa mwanachama.
(e) Kujiondoa mwenyewe au kujiuzulu.
(f) Kukiuka au kuvunja kwa makusudi kanuni zilizotungwa na CHAKAMWATA na kukaidi maonyo.

(2) Bila kuathiri Ibara 12(1) ya Katiba hii, Halmashauri zote za Wilaya zitathibitisha ukomo huo na kutoa taarifa ngazi za juu za uongozi wa chama.

(3) Hakuna mwanachama wa CHAKAMWATA atakayeruhusiwa kujiunga tena na CHAKAMWATA baada ya kuwa uanachama wake ulikoma kutokana na kuvunja Katiba na Kanuni za CHAKAMWATA kwa makusudi.

## SURA YA SITA

## SIFA ZA VIONGOZI WA CHAKAMWATA

**Sifa za kuwa Kiongozi wa CHAKAMWATA**

**13.**(1)(a)(i) CHAHAMWATA kitakuwa na viongozi mbalimbali katika ngazi zilizoainishwa katika Ibara 13 ya Katiba hii ambao watatumikia uongozi wao kwa muda wa miaka minne (4).

(ii) Kila mwanachama anayekidhi vigezo na sifa zitakazoainishwa hapa chini anaweza kuomba kuchaguliwa kuwa kiongozi wa CHAKAMWATA.

(iii) Ili kuwa kiongozi wa CHAKAMWATA, Mwombaji anapaswa awe na sifa zifuatazo:-

(a) Awe na usajili wa kudumu ndani ya CHAKAMWATA.

(b) Awe na akili timamu.

(c) Awe mwaminifu, mwadilifu na mwenye tabia nzuri kwa jamii husika.

(d) Awe na ajira ya kudumu au ya mkataba ndani ya nchi, kutoka serikalini, mashirika binafsi na watu binafsi.

(e) Asiwe amewahi kuhukumiwa na mahakama kwa ubadhirifu wa mali.

(f) Asiwe na tuhuma yoyote ya makosa ya jinai kwa wakati huo wa kuomba Uongozi.

(g) Awe na uzoefu na ujuzi katika kuhamasisha jamii juu ya mahusiano mazuri ya kikazi.

(h) Awe anaonyesha kufanikiwa katika uongozi.

(i) Awe tayari kutoa muda wake kwa ajili ya masuala ya wanachama wa CHAKAMWATA.

(j) Awe ni mwenye hekima na busara.

(k) Awe ni mwenye kupenda maendeleo na ustawi wa CHAKAMWATA.

(l) Awe na moyo wa kujitolea kufanya majukumu ya CHAKAMWATA bila kudai mshahara.

**Taratibu za kuchagua Viongozi wa CHAKAMWATA**

(b) Utaratibu wa kumpata kiongozi wa CHAKAMWATA katika ngazi yoyote ile utakuwa kama ulivyoainishwa katika kanuni za kudumu za CHAKAMWATA.

(i) Kutakuwa na matangazo ya wazi katika ngazi husika yatakayotolewa kwa wanachama wa CHAKAMWATA ili waweze kuomba nafasi ya uongozi.

(ii) Kila mwanachama mwenye sifa bila kujali jinsi, maumbile (ulemavu) au rangi atakuwa huru kuomba nafasi ya kuchaguliwa kwenye nafasi yoyote ya uongozi katika ngazi anayohitaji.

(iii) Fomu zote za kugombea uongozi zitaandaliwa na uongozi wa CHAKAMWATA Taifa na kupelekwa kwenye ngazi za chini.

(iv) Mgombea atachukua fomu na kuijaza kadiri itakavyohitajika kwenye fomu na kanuni za CHAKAMWATA.

(v) Kiongozi wa Kanda atalazimika kuomba fomu ya kugombea nafasi hiyo kwenye Ofisi ya CHAKAMWATA Taifa na kupigiwa kura na Mikoa na Halmashauri zilizopo katika Kanda yake. Kiongozi wa Mkoa atapigiwa kura na Halmashauri za mkoa wake.

(vi) Mgombea au Mwanachama yeyote ambaye hatakubaliana na matokeo ya uchaguzi na akiamini kuwa anazo sababu za

msingi na zenye ushahidi wa kutokubaliana na matokeo ya uchaguzi au jambo lolote lililoamriwa, ataruhusiwa kukata rufaa kwa kuzingatia Kanuni za CHAKAMWATA. **Kukata Rufaa dhidi ya Matokeo ya Uchaguzi.**

(2) (a) Kwa kuwa idadi kubwa ya Walimu inapatikana katika ngazi ya Kata na Halmashauri za Wilaya, uongozi na majukumu ya CHAKAMWATA yanajikita huko ili kuwa karibu na wanachama wake katika kushughulikia kero zao. **CHAKAMWATA Kuwa Karibu na Walimu.**

(b) Viongozi wa ngazi zote ndani ya CHAKAMWATA watalazimika kupewa posho itakayotokana na majukumu yao. Viwango vya posho kulingana na majukumu ya kila kiongozi kwa kila ngazi ya uongozi, vitaamuliwa na uongozi wa CHAKAMWATA Taifa na vitabadilika kulingana na wakati na uwezo wa chama kiuchumi. Hakutakuwa na mishahara isipokuwa vinginevyo, kwa maana ya kujitolea. Hakutakuwa na ajira za kudumu za viongozi ndani ya CHAKAMWATA isipokuwa kwa watumishi wa ofisi kama vile madereva, makarani, walinzi na wahudumu wengine. **Posho za Viongozi**

(c) Uongozi wa CHAKAMWATA utafuata mtindo au mfumo wa kutoka ngazi ya chini kwenda ngazi ya juu (Bottom-Up), ambapo wengi walio chini ndiyo wanaoongoza CHAKAMWATA badala ya wachache walio juu kuongoza peke yao. **Walimu kuongoza Chama**

### AJIRA KWA WAATUMISHI WASIO WALIMU

Kwa madhumuni ya kuboresha utendaji wa Chama na utoaji huduma kwa walimu, CHAKAMWATA kitaajiri watumishi wengine wasikuwa walimu kwa vigezo na sifa za kitaaluma na kiujuzi kama vile madereva, walinzi, makarani, n.k. na kuwapa mikataba ya ajira kwa mujibu wa sheria za nchi. Watumishi hao watapatikana kwa njia ya kuwateua, kuwachagua au kuwashindanisha katika usaili. **Maafisa wa Chama.**

### MUUNDO WA UONGOZI WA CHAKAMWATA

**Muundo wa Uongozi wa CHAKAMWATA**

(3) Sura ya Muundo wa uongozi wa CHAKAMWATA utakuwa na sehemu tatu au makundi matatu kama ifuatavyo:-

(a) Wajumbe wa Chama katika kila kituo cha kazi (shule au chuo)

(b) Viongozi waandamizi au Kamati Tendaji, ambao utakuwa na sura hii:-

- (i) Ngazi ya Kata
- (ii) Ngazi ya Halmashauri ya Wilaya
- (iii) Ngazi ya Kanda
- (iv) Ngazi ya Taifa

(c) Muundo wa viongozi wa Kamati mbalimbali

(i) Kamati ya Nidhamu; Ngazi ya Kata, Ngazi ya Halmashauri ya Wilaya na Ngazi ya Taifa.

(iv) Kamati ya Ukaguzi; Ngazi ya Kata, Ngazi ya Halmashauri ya Wilaya na Ngazi ya Taifa.

***UFAFANUZI WA MUUNDO WA VIONGOZI WAANDAMIZI WA CHAKAMWATA***

**Viongozi waanda Mizi wa CHAKAMWATA**

**14**. (1) Bila kuathiri Ibara 13 (3) ya Katiba hii, viongozi waandamizi ngazi ya Kata itakuwa na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu, Naibu Katibu na Mtunza Hazina.

(2) Bila kuathiri Ibara ya 13(3) ya Katiba hii, viongozi waandamizi ngazi ya Halmashauri ya Wilaya itakuwa na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu, Naibu Katibu na Mtunza Hazina.

(3) Bila kuathiri Ibara ya 13 (3) ya Katiba hii, kiongozi mwandamizi ngazi ya Mkoa atakuwa ni kiongozi mmoja tu atakayejulikana kama **"Mratibu wa Mkoa".**

Bila kuathiri Ibara ya 13 (3) ya Katiba hii, kiongozi mwandamizi ngazi ya (4) Kanda atakuwa ni kiongozi mmoja tu atakayejulikana kama **"Mratibu wa Kanda".**

(5) Bila kuathiri Ibara 13 (3) ya Katiba hii, viongozi waandamizi ngazi ya Taifa watakuwa na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu, Naibu Katibu na Mtunza Hazina.

**MGAWANYO WA KANDA ZA CHAKAMWATA ZA KIUONGOZI**

**Kanda za Kiuongozi Katika CHAKAMWATA**

(4) **(a)** Bila kuathiri Ibara 13(3) ya Katiba hii CHAKAMWATA utakuwa na mgawanyo wa Kanda kumi na moja kama ifuatavyo:-

(A) KANDA YA NYANDA ZA JUU: Itajumuisha Mikoa ya:-
- (i) Mbeya.
- (ii) Rukwa
- (iii) Katavi.

(B) KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI: Itajumuisha Mikoa ya:-
- (i) Iringa.
- (ii) Njombe.
- (iii) Ruvuma.

(C) KANDA YA KUSINI: Itajumuisha Mikoa ya:-
- (i) Mtwara.
- (ii) Lindi.

(D) KANDA YA KASKAZINI MASHARIKI: Itajumuisha Mikoa ya:-
- (i) Kilimanjaro
- (ii) Tanga

(E) KANDA YA KASKAZINI MAGHARIBI: Itajumuisha Mikoa ya:-
- (i) Arusha.
- (ii) Manyara.

(F)KANDA YA MASHARIKI: Itajumuisha Mikoa ya:-
- (i) Morogoro.
- (ii) Pwani.

(G) KANDA MAALUM: Itahusu Mkoa wa:-
(i) Dar-es-Salaam.
(H) KANDA YA ZIWA: Itajumuisha Mikoa ya:-
(i) Mwanza
(ii) Mara.
(iii) Geita.
(I) KANDA YA MAGHARIBI: Itajumuisha Mikoa ya:-
(i) Tabora.
(ii) Shinyanga.
(iii) Simiyu.
(J) KANDA YA ZIWA – MAGHARIBI: Itajumuisha Mikoa ya:-
(i) Kigoma.
(ii) Kagera.
(K) KANDA YA KATI: Itajumuisha Mikoa ya:-
(i) Dodoma.
(ii) Singida.
(iii) Uyui.

(4).(b) Waratibu wa CHAKAMWATA wa Mikoa ndiyo watakaoshughulikia mambo yote ya CHAKAMWATA kwenye ngazi ya Mkoa husika na watahakikisha kuwa umoja na mshikamano wa walimu ndani ya Mkoa na baina ya halmashauri za wilaya zinazounda Mkoa wake unakuwa hai na imara wakati wote.

(c) Waratibu wa CHAKAMWATA wa Kanda ndiyo watakaoshughulikia mambo yote ya CHAKAMWATA kwenye ngazi ya Kanda husika na watahakikisha kuwa umoja na mshikamano wa walimu ndani ya Kanda na baina ya Mikoa inayounda Kanda yake unakuwa hai na imara wakati wote.

## KAZI NA MADARAKA YA VIONGOZI WA CHAHAMWATA

## UFAFANUZI WA MAJUKUMU YA VIONGOZI WA KAMATI TENDAJI WA CHAKAMWATA

***Ufafanuzi wa kazi na Majukumu ya Viongozi waandamizi wa CHAKAMWATA***

**15.** Viongozi wa CHAKAMWATA wa ngazi yoyote kama ilivyoainishwa katika Ibara 13 ya Katiba hii watatekeleza majukumu yao inavyopaswa kwa mujibu wa Katiba hii na Kanuni zake

(1) **MWENYEKITI**: Kiongozi yeyote aliyetajwa kama Mwenyekiti katika ngazi yoyote ndani ya Katiba hii au kwa mujibu wa Ibara 13 ya Katiba hii atatekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:- **Mwenye kiti**

(a) Atakuwa Kiongozi Mkuu wa CHAKAMWATA katika ngazi husika.
(b) Atasimamia shughuli zote za CHAKAMWATA.
(c) Atakuwa msemaji na mtetezi mkuu wa CHAKAMWATA.
(d) Atakuwa mwenyekiti wa vikao vyote vya CHAKAMWATA katika ngazi anayohusika.
(e) Ataitisha mikutano mbalimbali ya CHAKAMWATA yeye mwenyewe au kupitia kwa Katibu.
(f) Atatoa msimamo na sera za CHAKAMWATA kama ilivyoamuliwa na vikao vya Taifa au ngazi husika.
(g) Atafuatilia utekelezaji wa maamuzi ya vikao vya CHAKAMWATA.

**Makamu Mwenye kiti**

(2) **MAKAMU MWENYEKITI**: Kiongozi yeyote aliyetajwa kama Makamu Mwenyekiti katika ngazi yoyote ndani ya Katiba hii au kwa mujibu wa Ibara 13 ya Katiba hii atatekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-
(a) Ataongoza vikao ikiwa Mwenyekiti hatakuwepo.
(b) Atakuwa msaidizi wa Mwenyekiti katika majukumu yote yanayomhusu Mwenyekiti.

**Katibu Mkuu/ Katibu**

(3) **KATIBU MKUU**: Kiongozi yeyote aliyetajwa kama Katibu au Katibu Mkuu katika ngazi yoyote ndani ya Katiba hii au kwa mujibu wa Ibara 13 ya Katiba hii atatekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-
(a) Atakuwa Mtendaji Mkuu wa shughuli za CHAKAMWATA.
(b) Ataratibu vikao vyote vya CHAKAMWATA kwa kuzingatia Katiba, Kanuni za chama.
(c) Atatunza kumbukumbu (Nyaraka) zote za CHAKAMWATA ambazo ni pamoja na:-
(i) Mihutasari ya vikao na Mikutano yote.
(ii) Hati za usajili wa CHAKAMWATA.
(iii) Orodha na takwimu za wanachama wa CHAKAMWATA
(iv) Mikataba na nyaraka mbalimbali zinazohusu CHAKAMWATA.
(v) Kitabu cha Wageni.
(vi) Atakuwa msemaji na mtetezi mkuu mwenza wa chama katika kutoa msimamo na sera pamoja na kukitetea CHAKAMWATA.

**Naibu Katibu Mkuu/ Naibu Katibu**

(4) **NAIBU KATIBU MKUU**: Kiongozi yeyote aliyetajwa kama Naibu Katibu au Naibu Katibu Mkuu katika ngazi yoyote ndani ya Katiba hii au kwa mujibu wa Ibara 13 ya Katiba hii atatekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-
(a) Atakuwa Msaidizi wa Katibu.
(b) Atafanyakazi zote zinazomhusu Katibu, ikiwa Katibu hatakuwepo.

(c) Atamsaidia Katibu kuandika kumbukumbu katika vikao na mikutano na kuzitunza.

**Mtunza Hazina**

(5) **MTUNZA HAZINA**: Kiongozi yeyote aliyetajwa kuwa Mtunza Hazina katika ngazi yoyote ndani ya Katiba hii au kwa mujibu wa Ibara 13 ya Katiba hii atatekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

(a) Atapokea fedha na Michango mbalimbali.
(b)Atandaa na kutoa taarifa sahihi za fedha katika vikao vya CHAKAMWATA.
(c) Atasoma bajeti.
(d) Atatunza vitabu vya fedha.
(e) Atatunza mahesabu yote ya CHAKAMWATA.
(f) Atabuni vyanzo mbalimbali vya mapato.

**Mratibu wa Mkoa**

(6) **MRATIBU WA MKOA**: Kiongozi yeyote aliyetajwa kuwa Mratibu wa Mkoa ndani ya Katiba hii au kwa mujibu wa Ibara 13 ya Katiba hii atatekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

(a) Atauwezesha Mkoa katika upashaji habari na taarifa kati ya uongozi wa Kanda na uongozi wa Halmashauri za Wilaya ndani ya Mkoa wake.
(b) Atakuwa Mshauri wa CHAKAMWATA ndani ya Mkoa wake.
(c) Atakuwa Mratibu wa mambo yote yanayohusu CHAKAMWATA ndani ya Mkoa wake.
(d) Atakuwa na uhuru wa kufanya vikao na viongozi wa Halmashauri za Wilaya ndani ya Mkoa wake kulingana na mazingira na jiografia ya Mkoa wake kwa kutoa taarifa ngazi ya Kanda kabla na baada ya Kikao husika.
(e) Atahakikisha kuwa umoja, mshikamano na ushirikiano wa walimu na viongozi wao ndani na baina ya Halmashauri za Wilaya zinazounda Mkoa wake unakuwa hai na imara wakati wote.
(f) Atawasaidia viongozi wa Halmashauri za Wilaya wa Mkoa wake katika kutimiza majukumu na kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili katika majukumu yao.

**Mratibu wa Kanda**

(7) **MRATIBU WA KANDA**: Kiongozi yeyote aliyetajwa kuwa Mratibu wa Kanda ndani ya Katiba hii au kwa mujibu wa Ibara 13 ya Katiba hii atatekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

(a) Ataiwezesha Kanda katika upashaji habari na taarifa kati ya uongozi wa Taifa na uongozi wa Mikoa ndani ya Kanda yake.
(b) Atakuwa Mshauri wa CHAKAMWATA ndani ya Kanda yake.
(c) Atakuwa Mratibu wa mambo yote yanayohusu CHAKAMWATA ndani ya Kanda yake.
(d) Atakuwa na uhuru wa kufanya vikao na viongozi wa Mikoa ndani ya Kanda yake kulingana na mazingira na jiografia ya Kanda yake kwa kutoa taarifa ngazi ya Taifa kabla na baada ya Kikao husika.
(e) Atahakikisha kuwa umoja, mshikamano na ushirikiano wa walimu na

viongozi wao ndani na baina ya mikoa inayounda kanda yake unakuwa hai na imara wakati wote.

(f) Atawasaidia viongozi wa Halmashauri za Wilaya wa Mkoa wake katika kutimiza majukumu na kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili katika majukumu yao.

**(8) MJUMBE KWENYE KITUO CHA KAZI (SHULE/CHUO)**

**Mjumbe wa Kituo cha Kazi (Chuo/ Shule)**

(a) Atakuwa mmoja tu na atachaguliwa na walimu wenzake shuleni au chuoni.

(b) Kazi yake kubwa ni kukusanya kero za walimu wenzake pammoja na taarifa mbalimbali za walimu kwa kadiri zitakavyohitajika na ngazi za juu za chama na kuziwasilisha kwenye uongozi wa Kata ambao unaitwa Tawi.

(c) Ataitisha na kuongoza vikao ili kutoa taarifa na maelekezo mbalimbali ya chama kwa walimu pamoja na kupokea na kujadili masuala mbalimbali yanayohusu haki na masilahi ya walimu kituoni kwao.

(d) kwenye taasisi kubwa kama vile shule za sekondari kubwa za bweni na vyuo vya ualimu na zenye wafanyakazi wengi (mf. **$35^{+}$**), mjumbe ataruhusiwa kuwateua wasaidizi wake kwa kadiri atakavvyoona inafaa kwa lengo la kuongeza na kuboresha ufanisi wa kazi ya chama.

## KAMATI TENDAJI ZA CHAKAMWATA

***Ufafanuzi wa Muundo wa Viongozi wa Kamati Tendaji***

**Aina za Kamati tendaji za CHAKAMWATA**

**16.** CHAHAMWATA kitakuwa na viongozi mbalimbali watakaowajibika kulingana na nafasi na nyadhifa walizonazo katika utakelezaji wa majukumu yao kikatiba.

(1) **MJUMBE KWENYE KITUO CHA KAZI (SHULE/CHUO)**
Atakuwa mmoja tu na atachaguliwa na walimu wenzake shuleni au chuoni, kama ilivyoainishwa katika ibara ya 15(8) ya katiba hii.

(2) **KAMATI TENDAJI NGAZI YA KATA**: Bila kuathiri Ibara 13 (3) ya Katiba hii, viongozi wa Kamati tendaji ngazi ya Kata watakuwa ni pamoja na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu, Naibu Katibu na Mtunza Hazina.

(2) **KAMATI TENDAJI NGAZI YA HALMASHAURI YA WILAYA**: Bila kuathiri Ibara 13 (3) ya Katiba hii, viongozi wa Kamati tendaji ngazi ya Halmashauri ya Wilaya watakuwa ni pamoja na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu, Naibu Katibu na Mtunza Hazina.

**(3) KAMATI TENDAJI NGAZI YA MKOA**: Katika ngazi ya Mkoa Mtendaji atakuwa ni "Mratibu" aliyeainishwa katika Ibara 13 ya Katiba

hii.

(4)**KAMATI TENDAJI NGAZI YA KANDA**: Katika ngazi ya Kanda Mtendaji atakuwa ni "Mratibu" aliyeainishwa katika Ibara 13 ya Katiba hii.

(5) **KAMATI TENDAJI NGAZI YA TAIFA**: Bila kuathiri Ibara 13 (3) ya Katiba hii, viongozi wa Kamati tendaji ngazi ya Taifa watakuwa ni pamoja na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu, Naibu Katibu na Mtunza Hazina

***Ufafanuzi wa kazi na Majukumu ya Viongozi Kamati tendaji wa CHAKAMWATA***

**Majukumu ya Viongozi wa Tendaji za CHAKAMWATA**

**17**. (1) Kwa mujibu wa Katiba hii Viongozi watendaji katika ngazi mbalimbali isipokuwa ngazi ya Mkoa na Kanda; watatekeleza majukumu yao kwa uhuru ambayo ni:-

(a) Kubuni mikakati mbalimbali ya kuboresha, kuendeleza na kukistawisha CHAKAMWATA.

(b) Kupokea na kutatua matatizo ya wanachama.

(c) Kuandaa bajeti ya CHAKAMWATA kwa kushauriana na Mtunza Hazina.

(d) Kuandaa na kutoa taarifa mbalimbali zilizo sahihi zinazohusiana na CHAKAMWATA.

(e) Kuwashirikisha wanachama katika kuandaa mipango kazi kwa mambo au shughuli zinazohitaji utekelezaji.

(f) Kuhudhuria warsha, mikutano, semina, ziara na vikao kwa ajli ya mambo yanayohusiana na CHAKAMWATA na Taifa kwa ujumla wake.

(g) Kuwashirikisha wanachama katika kupitia, kujadili na kufanya maamuzi juu ya mipango mbalimbali ya CHAKAMWATA.

(h) Kuandaa, kuitisha na kusimamia vikao, mihadhara na mikutano mbalimbali ya CHAKAMWATA.

**KAMATI YA NIDHAMU YA CHAKAMWATA**

*Ufafanuzi Kuhusu Muundo wa Kamati ya Nidhamu*

**Kamati ya Nidhamu ya CHAKAMWATA**

**18.**(1) Bila kuathiri Ibara 13(3) ya Katiba hii, wajumbe wa Kamati ya nidhamu ngazi ya Kata, ngazi ya Halmashauri ya Wilaya na ngazi ya Taifa watakuwa ni wale walioainishwa katika kanuni zinazotambuliwa na CHAKAMWATA kwa mujibu wa Ibara 1(3) ya Katiba hii.

(2) Kamati ya Nidhamu itakuwa na wajumbe tisa na itaongozawa na Mwenyekiti na Katibu watakaochaguliwa kutoka miongoni mwao.

**KAZI NA MADARAKA YA KAMATI YA NIDHAMU**

**19.** Kamati ya nidhamu, bila kuathiri sehemu yoyote ya Katiba hii itakuwa na majukumu yafuatayo:-

(a) Kupendekeza Kanuni za kudumu na kufanya Marekebisho yanayojiri na kuyapeleka kwenye Kamati ya Katiba na Kamati Kuu.
(b) Kutatua na kushauri migogoro yote inayohusiana na shughuli za CHAKAMWATA kati ya Viongozi wa CHAKAMWATA na wanachama wa CHAKAMWATA
(c) Kusimamia nidhamu kwa wanachama na Viongozi wa CHAKAMWATA.

**Madaraka ya Kamati ya Nidhamu**

## KAMATI YA UKAGUZI

*Ufafanuzi Kuhusu Muundo wa Kamati ya Ukaguzi*

**20.** Bila kuathiri Ibara 13(3) ya Katiba hii, Kamati ya Ukaguzi ngazi ya Kata, ngazi ya Halmashauri ya Wilaya na ngazi ya Taifa, itaundwa na wajumbe walioainishwa katika kanuni za CHAKAMWATAkwa mujibu wa Ibara 1(3) ya Katiba hii.

## KAZI NA MADARAKA YA KAMATI YA UKAGUZI

**Kamati ya Ukaguzi**

**21.**(1) Kwa mujibu wa Katiba hii na kwa kufuata Kanuni za kudumu za CHAKAMWATA shughuli zote zinazohusiana na uchunguzi na ukaguzi wa mapato/ fedha zitafanywa na Kamati ya Ukaguzi ikiongozwa na Mkaguzi wa ndani ambaye naye atahakikiwa na Mkaguzi wa nje. Mkaguzi wa nje aweza kutoka serikalini au mtu yeyote binafsi mwenye sifa na aliyesajiliwa na serikali.

**Madaraka ya Kamati ya Ukaguzi**

(2) Kamati ya Ukaguzi itawajibika kushughulikia haya:-
(a) Kukagua na kuchunguza ukweli wowote wa mapato/ fedha kulingana na ngazi husika zilizoainishwa katika Ibara 13 ya Katiba hii na kuwasilisha taarifa ya ukaguzi huo katika uongozi wa juu wa ngazi husika.
(b) Kupendekeza Maboresho ya Kanuni za kudumu kwa kushirikiana na Kamati ya Nidhamu, Kamati ya Katiba na Kamati kuu kwa mujibu wa Ibara 1(3) ya Katiba hii.
(c) Kupendekza adhabu mbalimbali dhidi ya wale waliothibitishwa kuwa ama ni wabadhirifu au wezi wa mali za CHAKAMWATA na kuziwasilisha kwenye Mkutano Maalum.
(d) Kutoa ushauri wa namna bora ya kutafuta vyanzo vya mapato, na kulinda mapato yaliyokusanywa pamoja na njia sahihi za kupanga matumizi yake.

## UKOMO WA UONGOZI WA CHAMA CHA CHAKAMWATA

***Ufafanuzi kuhusu Ukomo wa Uongozi wa CHAKAMWATA Kwa Ngazi Zote***

**22.** (1) Kwa kuwa CHAKAMWATA ni chama cha wafanyakazi ambacho si cha kujipatia faida na kila mwalimu atajiunga kwa hiari yake mwenyewe, hakutakuwa na ajira za kudumu kwa viongozi wa chama, na

kila kiongozi atafanyakazi kwa kujitolea na atalipwa posho badala ya mshahara. Kwa hiyo basi; Kwa mujibu wa Katiba hii kila kiongozi atatumikia kiti chake cha uongozi kwa muda wa miaka minne (4) na kisha anaweza kugombea na kuchaguliwa kwa mara nyingine kama wanachama watamuona kuwa anafaa.

**Kutumikia Uongozi wa CHAKAMWATA na Ukomo wake**

(2)Uchaguzi wa Viongozi wa CHAKAMWATA utafanyika tarehe itakayotangazwa na uongozi wa ngazi husika kila baada ya muda wa miaka minne (4) isipokuwa vinginevyo, ndipo utakapofanyika uchaguzi.

**Uchaguzi Mdogo wa Dharula**

(3) (a) Uchaguzi mdogo wa viongozi wa CHAKAMWATA pia unaweza kufanyika kwa dharula wakati wowote endapo:-

(i) Kiongozi mmoja wapo atafariki dunia.
(ii) Kiongozi mmoja wapo atapoteza sifa za kuwa kiongozi na kufukuzwa au kuondolewa katika uongozi kwa taratibu maalum.
(iii) Kiongozi mmoja wapo atajiuzulu kwa hiari yake mwenyewe.
(iv) Kiongozi mmoja wapo ataugua magonjwa sugu ya akili.
(v) Kiongozi mmoja wapo atahama eneo husika (mfano: Tawi) na kwenda mahali pengine.

(b) Endapo kiongozi atasimamishwa uongozi au kufukuzwa, uteuzi wa muda unaweza kufanyika ili kuziba pengo. Uteuzi huu utafanyika kwa kuzingatia kanuni za kudumu za CHAKAMWATA.

**Uteuzi wa Viongozi wa Muda**

**Mamlaka ya Walimu juu ya Viongozi wao**

(4) Mkutano Mkuu wa Kata na Wilaya unaweza kuthibitisha maamuzi ya kuondolewa kwa uongozi/kiongozi yeyote. Iwapo imefanyika hivyo katika ngazi za chini, basi taarifa zitatolewa kwenye ngazi ya juu. Ikiwa imefanyika hivyo kwenye ngazi za kati, basi taarifa itatolewa kwenye ngazi za chini na ngazi za juu yake na ikiwa imefanyika hivyo kwenye ngazi ya Taifa basi taarifa itatolewa kwenye ngazi zote za chini.

Kiongozi wa Mkoa anaweza kuondolewa kutokana na tuhuma zilizothibitishwa na Wilaya za Mkoa husika na uthibitisho wa kuondolewa kwake utafanywa na uongozi wa Kanda na kutoa taarifa kwenye ngazi za juu na chini.

(5) Kiongozi wa Kanda anaweza kuondolewa kutokana na tuhuma zilizothibitishwa na Mikoa ya Kanda husika na uthibitisho wa kuondolewa kwake utafanywa na uongozi wa Taifa na kutoa taarifa kwenye ngazi za Mikoa na Wilaya.

(6) Kiongozi yeyote wa CHAKAMWATA-Taifa anaweza kuondolewa madarakani baada ya tuhuma zitakazothibitishwa na Mkutano Mkuu wenye wajumbe kutoka katika Halmashauri, Mikoa na Kanda mbalimbali.

(7) Utaratibu, vigezo na sababu zitakazotumika kuwaondoa viongozi madarakani ndizo zitakazotumika kuwaondoa maafisa wengine wa chama walioajiriwa.

walemavu (kama wapo) kwa kila Wilaya, wawakilishi wawili wa walimu ngazi ya Mkoa kwenye mkutano wa Taifa pammoja na Mratibu wa Mkoa husika.
(f) Bila kuathiri Ibara nyingine yoyote ya Katiba hii, Mkutano Mkuu wa Mkoa utakuwa ndicho chombo na sauti kuu ya walimu ndani ya Mkoa husika kuhusu ajira, wajibu, haki, kero na maslahi ya wafanyakazi na hatua za kuchukua dhidi ya mwajiri/ waajiri wao endapo italazimika kufanya hivyo.

(g) Katika ngazi ya Taifa Mkutano Mkuu utakuwa na wajumbe ambao ni:-

(i) Viongozi wote wa Kitaifa.
(ii) Viongozi wote wa Halmashauri za Wilaya nchini.
(iii) Mratibu mmoja kutoka kila Mkoa.
(iv) Mratibu mmoja kutoka kila Kanda.
(v) Muwakilishi mmoja wa walemavu kutoka kila Mkoa.
(vi) Muwakilishi mmoja wa walemavu kutoka kila kanda.
(vii) Wawakilishi wawili wa walimu kutoka kila Mkoa.

**(h)** Bila kuathiri Ibara nyingine yoyote ya Katiba hii, Mkutano Mkuu wa Taifa utakuwa ndicho chombo na sauti kuu ya walimu nchini kuhusu ajira, wajibu, haki, kero na maslahi ya wafanyakazi na hatua za kuchukua dhidi ya mwajiri/ waajiri wao endapo italazimika kufanya hivyo.

(i) Bila kuathiri Ibara nyingine yoyote ya Katiba hii, Kamati tendaji ya Kata, Halmashauri ya Wilaya, Mkoa na Taifa, wanaweza kwa niaba ya Mkutano Mkuu wa ngazi husika na kwa kupitia vikao, kutoa matamko na msimamo wa walimu kuhusu ajira, wajibu, haki, kero na maslahi ya walimu na hatua za kuchukua dhidi ya mwajiri/ waajiri wao endapo italazimika kufanya hivyo.

## KAZI ZA MKUTANO MKUU WA CHAKAMWATA

**Kazi na Majukumu ya Mikutano Mbalimbali ya CHAKAMWATA**

(2) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CHAKAMWATA katika kila ngazi zilizoainishwa katika Ibara 13 ya Katiba hii, pamoja na mambo mengine basi watalazimika kufanyakazi ya:-

(a) Kuzitambua kero, haki na masilahi halali ya walimu katika ujumla wake.
(b) Kujadili juu ya ukandamizaji, unyanyasaji, dhuluma na uonevu wowote unaofanywa na mwajiri/waajiri dhidi ya walimu na kupanga namna ya kukabiliana nao.
(c) Kufanya maamuzi juu ya hatua za kuchukua dhidi ya mwajiri/waajiri ili kudai haki na masilahi ya walimu baada ya

mazungumzo ya kawaidi kushindikana, au makubaliano yoyote yaliyokuwa yamefikiwa hapo awali, kukiukwa na mwajiri/waajiri au kuhusu sheria na sera yoyote kandamizi ambayo waajiri/mwajiri ataitunga na kuitekeleza bila kuridhiana na walimu kupitia CHAKAMWATA.

(d) Kusoma bajeti ya mapato na matumizi ya CHAKAMWATA.

(e) Kupitisha bajeti ya mapato na matumizi ya CHAKAMWATA.

(f) Kupokea na kujadili Taarifa mbalimbali za CHAKAMWATA

(g) Kufanya tathmini mbalimbali za maendeleo ya CHAKAMWATA.

(h) Kuwajadili na kutoa maamuzi/ maonyo kwa wanachama na Viongozi wa CHAKAMWATA wanaokwenda kinyume na taratibu za CHAKAMWATA kama watapokea kutoka kwenye Kamati ya Nidhamu.

(i) Kujadili namna na kutoa mapendekezo kama kuna haja ya kujiunga/kujitoa kwenye muungano wa vyama vingine vya wafanyakazi au shirikisho la vyama vya wafanyakazi(affiliation or amalgamation to other Trade Union {s}or to federation of trade unions)

(j) Kupiga kura za kutangaza mgogoro au mgomo katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya, Mkoa au ngazi ya Taifa dhidi ya mwajiri endapo mazungumzo ya kudai haki na maslahi halali yatashindwa kufikia muafaka.

(k) Hatua za kisheria za kutangaza mgogoro au mgomo dhidi ya mwajiri zitaendelea kufuatwa na kutekelezwa.

(3) Kazi za Mkutano Mkuu wa CHAKAMWATA Taifa pamoja na kazi hizo zilizoainishwa hapo juu katika Ibara ya 24(2) ya Katiba hii wajumbe watalazimika kujadili na kupitisha marekebisho (Amendments) ya Katiba ya CHAKAMWATA na Kanuni zake iwapo ni lazima kufanya hivyo.

(4) Mkutano Mkuu wa CHAKAMWATA Taifa, pamoja na kazi zingine zilizoainishwa hapo juu katika Ibara hii utakuwa ndicho chombo na sauti ya mwisho kwa makosa mbalimbali yaliyoletwa kupitia Kamati tendaji ya Nidhamu na kutoa hatima yake.

(5) Mkutano Mkuu wa CHAKAMWATA Taifa utakuwa ndicho chombo na sauti ya mwisho juu ya mambo yanayohusu ajira, haki na maslahi ya walimu na hatua za kuchukua dhidi ya mwajiri/ waajiri katika ngazi ya kitaifa, endapo italazimika kufanya hivyo.

## KUITISHA NA KUENDESHA MGOMO
## MAENEO YA KUFANYIWA MGOMO NA CHAKAMWATA

**Kudai Haki na Masilahi kwa Mgomo**

**25.** (1) Kwa kuwa wazalishaji sugu wa kero za walimu nchini ni waajiri naq wawakilishi wa waajiri wali karibu na walimu, na bila kuathiri ib**ara**

**ya** 24(2)(a-c, j-k) ya Katiba hii, na ikiwa mazungumzo ya kawaida kati ya CHAKAMWATA na waajiri au wawakilishi wa waajiri katika maeneo hayo hayataleta tija, basi CHAKAMWATA kitawaongoza walimu kuitisha na kufanya mgomo dhidi ya mwaji au mwakilishi wa mwajiri katika maeneo yafuatayo.

(i) Mgomo katika ngazi ya kituo cha dhidi ya uongozi wa kituo hicho endapo mwajiri au kiongozi wa taasisi anayemwakilisha mwajiri anafanya dhuluma, unyanyasaji na ukandamizaji kwa walimu na mazungumzo ya kawaida yameshindikana. Kabla ya kufanya mgomo huo, ni sharti mjumbe wa chama awasiliane na uongozi wa Kata au Wilaya kwa nia ya kuandaa na kufuata taratibu stahiki za mgomo.

(ii) Mgomo katika ngazi ya Kata; kama walimu ndani ya eneo la kata wanapata kero zinazosababishwa na mwajiri au mwakilishi wa mwajiri katika kata na ikiwa mazungumzo ya kawaida na kiongozi huyo hayajaleta tija, basi walimu kwa kuongozwa na CHAKAMWATA wanaweza kuitisha mgomo ili kufikisha ujumbe wa kudai haki na masilahi yao.

(iii)Mgomo katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya; Ikiwa mwajiri au mwakilishi wa mwajiri katika Halmashauri ya Wilaya hatendi haki kwa walimu kwa kuwanyanyasa, kuwapuuza, kuwadharau, kutowapandisha madaraja kwa wakati ua kuwapandisha kwa upendeleo, kudhulumu hali na maslahi yao mbalimbali, na kama mazungumzo ya kawaida kuhusu ukiukwaji huo wa haki na masilahi ya walimu hayajaleta tija, basi CHAKAMWATA kitawaongoza walimu na kuitisha mgomo dhidi ya mwajiri au mwakilishi huyo wa mwajiri.

(iv) Mgomo katika ngazi ya Mkoa; Ikiwa mwajiri au mwakilishi wa mwajiri katika ngazi ya Mkoa hatendi haki kwa walimu kwa kuwanyanyasa, kuwapuuza, kuwadharau, kutowapandisha madaraja kwa wakati ua kuwapandisha kwa upendeleo, kudhulumu hali na maslahi yao mbalimbali, na kama mazungumzo ya kawaida kuhusu ukiukwaji huo wa haki na masilahi ya walimu hayajaleta tija, basi CHAKAMWATA kitawaongoza walimu na kuitisha mgomo dhidi ya mwajiri au mwakilishi huyo wa mwajiri kwa nia ya kudai haki na masilahi yao yanayodhulumiwa, kupunjwa au kupuuzwa.

(vi) Mgomo katika ngazi ya Taifa; Ikiwa mwajiri wa walimu katika ngazi ya Taifa hatendi haki kwa walimu kwa kuwanyanyasa, kuwapuuza, kuwadharau, kutowapandisha madaraja kwa wakati ua kuwapandisha kwa upendeleo, kudhulumu hali na maslahi yao mbalimbali au kutunga sheria na sera zinazowakandamiza walimu na kama mazungumzo ya kawaida kuhusu ukiukwaji huo wa haki na masilahi ya walimu hayajaleta tija, basi CHAKAMWATA kitawaongoza walimu na kuitisha mgomo wa nchi nzima dhidi ya mwajiri kwa nia ya

kupinga ukandammizaji huo na kudai haki na masilahi yao.

## SURA YA NANE

### BODI YA WADHAMINI WA CHAKAMWATA

**Bodi ya Wadhamini**

**25.**(1) Kutakuwa na Bodi ya wadhamini wa CHAKAMWATA.

(2) Bodi ya wadhamini itakuwa kama ilivyotafsiriwa katika Ibara ya 5(1) ya Katiba hii.

(3) Bodi ya wadhamini itaundwa na Wajumbe wasiozidi watano.

**Upatikanaji wa Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini**

**26.**(1) Wajumbe wa Bodi watapatikana kupitia uteuzi utakaofanywa na Vikao vya Kamati Tendaji ya Taifa na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa Taifa.

(2)Baada ya kuthibitishwa na kutangazwa, wajumbe hao wa Bodi watakuwa na Mamlaka kamili ya kufanyakazi kama wajumbe wa Bodi ya CHAKAMWATA.

(3) Bodi ya Wadhamini itakuwa na Mwenyekiti na Katibu wake na wengine watakuwa wajumbe ndani ya Bodi hiyo.

**27.**(1) Wajumbe wa Bodi akiwemo Mwenyekiti watakuwa na haja ya kukidhi vigezo vitakavyopendekezwa kwenye vikao vya Kamati.

(2) Iwapo mjumbe wa Bodi amefariki, amejiuzulu, amefukuzwa au amehama makazi na kwenda kuishi nje ya nchi, basi Kamati tendaji ya Taifa inaweza kujadili na kupendekeza namna nzuri ya kuziba pengo hilo na kupeleka maoni yao kuthibitishwa kwenye Mkutano Mkuu.

### VIKAO VYA BODI YA WADHAMINI

**Vikao vya Bodi ya Wadhamini**

**28.** (1) Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini watakaa mahali popote ndani ya nchi na kufanya vikao kulingana na hoja zotakazokuwepo.

(2) Wajumbe wa Bodi watakaa kikao kimoja kwa mwaka. Wanaweza kukaa kikao zaidi ya kimoja iwapo kuna jambo la dharula linalogusa maslahi ya CHAKAMWATA.

(3) Ni lazima taarifa itolewe kwanza kwa Kamati tendaji ya Taifa ndipo Kikao cha dharula cha Bodi ya Wadhamini kikae kwa jambo la Dharula.

(4) Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini kwa kumtumia katibu wake, ndiye atakayekuwa na mamlaka ya kuitisha vikao vya Bodi ya Wadhamini.

(5) Muundo wa vikao vya Bodi ya Wadhamini utakuwa sawia na vikao Vingine kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni za kudumu za CHAKAMWATA.

### KAZI ZA BODI YA WADHAMINI

**Shughuli na Wajibu wa Bodi ya Wadhamini**

**29.**(1) Bodi ya Wadhamini itakuwa ndiyo washauri wakuu wa

CHAKAMWATA

(2) Bodi ya Wadhamini itakuwa ndiyo chombo na nguzo pekee ya Mikopo ya CHAKAMWATA.

(3) Bodi ya Wadhamini itakuwa ndicho chombo kikubwa cha Kulinda mali za CHAKAMWATA.

(4) Bodi ya Wadhamini itakuwa ndicho chombo pekee cha kutetea, kulinda na kusimamia maslahi ya CHAKAMWATA dhidi ya mamlaka zingine.

**UKOMO WA KUWA MJUMBE WA BODI YA WADHAMINI**

**Ukomo wa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini**

**30.**(1) Mjumbe wa Bodi ya wadhamini atakuwa amekosa sifa za kuwa mjumbe iwapo itathibitika na wajumbe wa Mkutano Mkuu Taifa kuwa amekiuka kiapo cha udhamini wa CHAKAMWATA.

(1) Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini anaweza kukoma kuwa mjumbe wa Bodi ya Wadhamini kwa kujiuzulu mwenyewe, iwapo mjumbe wa Bodi amefariki, amefukuzwa au amehama makazi na kwenda kuishi nje ya nchi,

(3)Bila kuathiri 29(1) ya Katiba hii, Mkutano Mkuu utatoa mapendekezo na kuhakikisha kuwa ameteuliwa mdhamini mwingine atakayeziba pengo hilo.

## SURA YA TISA

## MFUKO MKUU, FEDHA NA VYANZO VYA MAPATO YA CHAKAMWATA

**31.**(1) Mambo yote yanayohusu fedha na mali za zingine za CHAKAMWATAvitatunzwa kwenye mfuko mkuu wa CHAKAMWATA.

(2) Namna nzuri ya utunzaji wa fedha na mali itaainishwa kwenye Kanuni za kudumu za CHAKAMWATA.

(3) Ni marufuku kufuja mali, kutunza nje ya mfuko kwa visingizio visivyokuwa na msingi vinavyoweza kusababisha upotevu wa mali na /fedha za CHAKAMWATA.

(4) Mtunza Hazina atawajibika na kuhakikisha kwamba mali zote/fedha zimetunzwa mahali salama ndani ya mfuko mkuu.

**VYANZO VYA MAPATO YA CHAKAMWATA**

**Vyanzo vya Mapato na Utunzaji Wake**

**32.** (1) Vyanzo vya Mapato ya CHAKAMWATA vitakuwa ni:-

(i) Michango ya wanachama ya kila mwezi ambayo ni **1%** ya mshahara wake wa kila mwezi.

(ii) Michango midogomidogo kutokana na harambee.

(iii) Misaada kutoka kwa Wafadhili/Wahisani watakaojitokeza.

(iv) Miradi na uwekezaji kwenye vitega uchumi kama vitakuwepo.
(v) mauzo ya mali au faida kutoka katika miradi kama itakuwepo.
fedha na mali zinginezo zitachangwa na kukabidhiwa kwa Mtunza Hazina kisha ataziweka kwenye mfuko mkuu.

## UTUNZAJI NA MATUMIZA YA FEDHA NA MALI ZA CHAKAMWATA

### UTUNZAJI WA FEDHA NA MALI ZA CHAKAMWATA

**Utunzaji wa Fedha na Mali za CHAKAMWATA**

**33.** (1) Mfuko wa kutunzia fedha itakuwa ni Benki iliyotambulishwa na Kukubaliwa na wanachama wa CHAKAMWATA.
(2) Waweka saini katika akaunti inayotambuliwa na CHAKAMWATA hawatazidi wajumbe wanne.
(3) Namna nzuri ya kutoa fedha/ kuchukua fedha kwenye akaunti ya CHAKAMWATA itaainishwa kwenye Kanuni za kudumu za CHAKAMWATA.
(4) Katibu wa CHAKAMWATA wa ngazi husika atakuwa ndiye Mtunzaji mkuu wa mali za CHAKAMWATA zisizohamishika na zinazohamishika.

**Benki**

(5) Fedha zote za CHAKAMWATA zitatunzwa Benki.

### MATUMIZI YA FEDHA NA MALI ZA CHAKAMWATA

**Matumizi ya fedha za CHAKAMWATA**

**34.** (1) Mapato yote yatatumika kuendeleza CHAKAMWATA
(2) Bila kuathiri Ibara ya 33(1) ya Katiba hii fedha zote zitatumika ikiwa ni pamoja na gharama za machapisho, gharama za utafiti, posho za vikao kama ni lazima, mishahara ya wahudumu ambao siyo walimu iwapo watakuwepo, gharama za uendeshaji wa Ofisi, safari na posho za viongozi katika kutekeleza majukumu ya chama, safari na posho za wadhamini wakati wa vikao vyao, gharama za ukaguzi wa vitabu vya fedha, kulipia mapango ya ofisi, kununulia viwanja na kujenga miundombinu mbalimbali,kulipa mishahara ya wahuhumu na maafisa wa chama, Gawio la wanachama wa CHAKAMWATA kutoka kwenye vitega uchumi na miradi inayojiendesha kwa mafanikio kama itakuwepo, marejesho ambayo ni BONUS au shukurani kwa wanachama wa CHAKAMWATA wanaostaafu au kuacha kazi, Bonus hiyo itakuwa ni 50% ya michango ya mwanachama kwa maisha yake yote ya uanachama akiwa mtumishi na malipo mengine halali kwa mujibu wa matakwa ya wanachama wa CHAKAMWATA na sheria za nchi.
(3) Namna nzuri zaidi ya Matumizi ya fedha yataainishwa kwenye Kanuni za kudumu za CHAKAMWATA.

## SURA YA KUMI

### MAREKEBISHO YA KATIBA NA KANUNI MBALIMBALI ZA CHAKAMWATA.

**Namna ya kurekebisha Katiba na Maamuzi ya Marekebisho ya Katiba**

**35.** Katiba hii siyo **Maandiko ya Biblia Takatifu** wala **Msahafu wa Quran Tukufu.** Hivyo basi marekebisho ya Katiba hii pamoja na Kanuni zake yanaweza kufanyika wakati wowote kwa matakwa ya wanachama wa CHAKAMWATA wenyewe na kwa manufaa ya wanachama wote wa CHAKAMWATA.

**37.**(1) Hoja za Marekebisho ya Katiba zitajadiliwa kwenye vikao mbalimbali.

(2) Bila kuathiri masharti ya Katiba hii kila Mwanachama atakuwa na haki ya kushiriki mjadala wa marekebisho ya Katiba kupitia vikao vya ngazi kituo cha kazzi na ngazi ya Kata.

**38.** (1) Baada ya Majadiliano na Maridhiano Mkutano Mkuu utapitisha maamuzi ya marekebisho ya Katiba na Kanuni zake.

(2) Baada ya maamuzi ya marekebisho ya Katiba, basi itatangazwa kuwa baadhi ya vifungu vimefanyiwa marekebisho na pia ni lazima kumbukumbu zinazoonyesha mapitio hayo zitunzwe kwenye kumbukumbu maalum.

### KUFUTWA KWA CHAMA CHA CHAKAMWATA

**Kufutwa kwa Chama**

**39.** (1) Kwa kuwa Maisha na shughuli za Binadamu ni endelevu na yanakwenda kwa kurithishana kutoka kizazi kimoja kwenda kizazi kingine, ndivyo maisha na changamoto za walimu zilivyo pia.
Kwa mantiki hiyo basi, walimu hatukusudii kuwa itatokea siku sisi wenyewe tukaamua kukifuta CHAKAMWATA.

(4) Hata hivyo CHAKAMWATA kinaweza kikafutika chenyewe kiasilia (Natural disappearance) kutokana na sababu mbalimbali kama vile:-

(i) Kukosa wanachama wapya wanaojiunga wakati wanachama waanzilishi wanafariki na kustaafu.

(ii) Kushindwa kukidhi matarajio ya walimu na hivyo wanachama wake kujitoa wote.

(i) Kutokana na vuguvugu la mageuzi mapya na hivyo chama kubadilika kutokana na kuungana na vyama vingine na kuunda chama kimoja, n.k.

(2) Aidha, kutokana na sababu mbalimbali, kama mamlaka za nchi zitaamua kukifuta chama kwa sababu ama kitakuwa kimekiuka Katiba yake, Katiba na sheria za nchi kwa kiasi kikubwa au kwa sababu nyingine

yoyote ile na kwamba kosa au makosa hayo yatakuwa yamethibitishwa na vyombo vya kisheria, basi mambo yafuatayo yatalazimika kufanyika:-

(i) Bodi ya wadhamini na wajumbe wa Mkutano Mkuu watakaa kwa kila ngazi ili kujadili namna ya mgawanyo wa mali utakavyokuwa kabla ya kufuta chama kwa kuzingatia sheria za nchi.

(iii) Mgawanyo wa mali umefanyika vema na kila mwanachama amepata haki yake.

(iv) Maridhiano ya maamuzi yamefanyika kwa kila eneo na kila jambo linalohusu mali iliyoshindikana kugawanyika, na kuwa itabaki na itakuwa katika umiliki gani.

**Akidi ya Maamuzi ya Kukifuta Chama**

(3) CHAKAMWATA kitahesabika kuwa kimefutwa baada ya majadiliano ya wajumbe wa Mkutano Mkuu na maamuzi kuafikiwa kwa kura ya maandishi. Kura zitakazoonyesha kuwa haya ndiyo maamuzi ya kufuta chama hayatapungua/ hazitapungua kura theluthi mbili ya wajumbe halali wa Mkutano Mkuu watakaohudhuria katika mkutano wa maamuzi hayo.